BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Nne – Tarehe 15 Mei, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2017/2018.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

72. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alifanya ziara nchini Indonesia wakati Makamu wa Pili wa Rais amefanya ziara nchini India.

Je, wananchi wategemee neema gani baada ya ziara hizo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

69. Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Jimbo Paje) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika soko la samaki la Darajani kumekuwa na tozo ya shilingi 400/= kila siku kwa wafanyabishara wa eneo hilo. Hata hivyo licha ya tozo hilo, mazingira ya soko siyo ya kuridhisha na Wizara imeshindwa kufanya matengenezo ya maeneo ya kuuzia na kuhifadhia samaki pamoja na kuweka usafi nje na ndani.

(a) Mkakati gani umewekwa kufanya matengenezo ya soko la samaki Darajani ndani na nje.

(b) Tozo wanazotozwa wafanyabiashara hao ya shilingi 400/= kila siku zinatumika vipi wakati eneo la soko hilo ni chafu.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

138. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Chukwani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Kwa kuwa Serikali katika mipango yake imeweka kipaumbele katika suala zima la michezo hususan katika skuli zetu.

Je, kuna taratibu gani zilizopangwa kwa masuala ya maslahi pamoja na usafiri kwa maofisa wanaofuatilia masuala ya michezo.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

141. MHESHIMIWA DKT. MWINYIHAJI MAKAME MWADINI (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Shirika la Habari (ZBC) kwa muda mrefu lilikuwa likirusha taarifa ya “hali ya hewa kwa masaa 24” kila siku baada ya taarifa ya habari ya saa 2 na robo usiku. Taarifa hiyo hutayarishwa na watu wa Hali ya Hewa, Uwanja wa Ndege wa Karume.

(a) Nini sababu za msingi zilizopelekea taarifa hizo kutorushwa hewani na ZBC - TV ilhali watu wa hali ya hewa wanazitayarisha na wanazo.

(b) Huoni ZBC – Radio kukataa kurusha taarifa hizo haiwatendei haki wakulima, wakwezi na wavuvi wa Zanzibar kinyume na malengo ya kuanzishwa ZBC - TV ya kuwapa habari na kuwaelimisha wananchi.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

67. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa kuwa kwenye eneo la Uwekezaji huko Fumba kuna mpango wa kujenga “Ferry Terminal” ili kurahisisha usafiri wa baharini kati ya Zanzibar na Dar es Salaam jambo ambalo litasaidia na kupunguza msongamano mkubwa kwenye bandari ya Malindi na kuharakisha usafiri huo wa kwenda na kurudi Dar es salaam.

(a) Je, Serikali bado ina mpango wa kujenga “Ferry Terminal” katika eneo hilo.

(b) Kama upo, ni lini ujenzi huo unatarajiwa kuanza ili kwenda sambamba na ujenzi wa mji ambapo baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, wakaazi wa mji huo na Zanzibar kwa ujumla wataweza kutumia “Ferry Terminal” hiyo.

68. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Mnamo tarehe 23/3/2017, Televisheni ya Shirika la Habari Zanzibar (ZBC) ilimnukuu Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Idd akiwa safarini kuelekea India, akisema kuwa Zanzibar ina uhaba wa ardhi na akapendekeza mpango wa makaazi uwe wa nyumba za ghorofa ili familia nyingi ziweze kuishi katika eneo dogo.

(a) Mapendekezo haya mazuri yaliyotolewa na Kiongozi wetu yapo katika mpango gani wa kutekelezwa ili kukabiliana na uhaba wa ardhi.

(b) Yapo baadhi ya maeneo yanajengwa nyumba za ghorofa lakini ruhusa inatolewa mwisho ghorofa mbili tu, je, kweli Serikali ipo tayari kukabiliana na tatizo la uhaba wa ardhi.

(c) Serikali ipo tayari kuruhusu ujenzi wa ghorofa zaidi ya mbili kwa maeneo yote ili kutekeleza kwa vitendo rai za viongozi wetu wakuu.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

9 MHESHIMIWA SALHA MOHAMED MWINJUMA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Hivi karibuni tumeshuhudia uchaguzi wa Viongozi wa Kitaifa wa Baraza la Vijana Zanzibar, lakini mpaka leo hatujui walipo na wanafanya shughuli gani, kwa kukosa eneo kwa ajili ya utendaji wa shughuli zao kama makao makuu yao.

Je, ni lini Serikali itawapatia Ofisi Vijana wake ili kuweza kuwa na Makao Makuu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
15 Mei, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.